**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# MWONGOZO WA KUMFUATILIA MTU ALIYEKUWA KARIBU NA MGONJWA (CONTACT) WA COVID-19

**Toleo la Pili Tarehe 26 Mei, 2020**

## 1. UTANGULIZI

Ugonjwa wa Coronavirus 2019 (COVID-19) ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na kirusi cha coronavirus 2 (SARS-CoV-2). Ugonjwa huo umeenea ulimwenguni kote kutoka Desemba 2019 hadi sasa na kusababisha janga la ulimwengu. Virusi huenea kutoka kwa mtu mmoja kwenda mwingine kwa kuingiwa na majimaji kutoka kwa mtu mwenye maambukizi wakati wa kukohoa, kupiga chafya au kuongea. Aidha, watu wanaweza kuambukizwa kwa kugusa mazingira au vitu vilivyogusana na majimaji kutoka kwa mtu aliyeambukizwa na kujigusa sehemu za pua, mdomo au macho.

Moja ya hatua muhimu ambazo Shirika la Afya Duniani (WHO) limependekeza kwa nchi wanachama kama moja ya njia kuu za kuzuia maambukizi yasisambae ni kuweza kuhakikisha kuwa watu waliokuwa karibu na mgonjwa wanafuatiliwa (Contact Tracing). Lengo ni kuhakikisha iwapo watu hawa watapata dalili za awali za ugonjwa wa COVID-19, hawaambukizi watu wengine na vile vile, hatua na huduma stahiki ikiwa ni pamoja na matibabu zinatolewa kwa haraka.

Mwongozo huu umeandaliwa kuwawezesha watoa huduma kuwafuatilia kwa ukamilifu watu ambao watakuwa wamejitenga nyumbani au kwenye makazi maalum ***(Self Quarantine at Home or Designated Residency),*** kwa kuzingatia masharti ambayo yapo katika kiambatisho **A**. Watu watakaofuatiliwa katika makazi maalum, ni wale ambao wameridhia

wenyewe kwenda sehemu mbali na nyumbani kwa ajili ya kujitenga, au ni wale ambao tathmini ya watoa huduma itaonesha kuwa hawawezi kukaa nyumbani. Aidha, watu hao watahusika wenyewe kujilipia gharama za kujitenga. Ikiwa "contacts" wako kwenye taasisi na kambi, na makazi maalum, timu za afya za Mikoa na Halmashauri zikishirikiana na uongozi wa taasisi husika zifanye tathmini na kuweka utaratibu wa kuwawezesha contacts kuendelea na masomo/shughuli zao wakizingatia njia madhubuti za kujikinga.

**Katika mwongozo huu, mtu aliyekuwa karibu na mgonjwa (contact) ni yule ambaye alikuwa karibu (chini ya mita 1) na mgonjwa aliyethibitika kuwa na COVID-19 kuanzia siku mbili kabla mgonjwa hajaanza kuonesha dalili.** Mtu huyu atakuwa anafuatiliwa nyumbani mara ya kwanza ili kufanya tathmini ya mahali anapoishi na kupewa elimu ya umuhimu wa kujitenga yeye na wanaoishi naye **(Kiambatanisho A)**. Aidha, "contact" atafuatiliwa kila siku kwa siku zisizopungua 14 kwa muktadha wa Udhibiti wa Ugonjwa wa COVID-19. Mwongozo huu utekelezwe kwa ushirikiano wa pamoja kati ya "contact" anayefuatiliwa, wataalamu wa afya, ustawi wa jamii na uongozi wa Serikali za Mitaa na taasisi husika.

Mwongozo huu utatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 ambayo ukiukwaji wake utapelekea kuchukuliwa hatua kali. Kabla ya kuanza kufuatiliwa "contact" atasoma na kutia saini fomu ya kuzingatia masharti ya kujitenga **(Kiambatanisho B).**

## 2. MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UFUATILIAJI WA CONTACTS

### 2.1 Timu ya usimamizi wa ufuatiliaji kwa mtu aliyekuwa karibu na mgonjwa katika ngazi ya Wilaya/Halmashauri

Timu hii itasimamiwa na Mkuu wa Wilaya, na kupewa utaalam na Mganga Mkuu wa Wilaya. Aidha wajumbe wa Kamati hii ni pamoja na DAS, DED, DSO, na DHO/Epidemiologist pamoja na wengine watakaoonekana wanahusika.

Kamati hii itasimamia zoezi la ufuatiliaji wa Contacts ikiwa ni pamoja na;

- Kupokea taarifa juu ya utekelezaji wa zoezi la ufuatiliaji na kutolea maamuzi masuala yenye changamoto
- Kuandaa na kuitisha vikao ili kujadili mikakati ya utekelezaji
- Kuhakikisha inaunda timu ya watalaam katika kutekeleza zoezi hili na kuwawezesha wataalam kuwa na vifaa kinga, rasilimali fedha na usafiri kwa ajili ya zoezi la ufuatiliaji

## 2.2 Vitendea Kazi vya Wafuatiliaji

a. Rejista ya watu waliokuwa karibu na mgonjwa
b. Fomu ya orodha ya watu waliokuwa karibu na mgonjwa wa CORONA (Contact Listing Form)
c. Fomu ya ufuatiliaji wa kila siku (Daily Contact Follow Up form)
d. Fomu ya kutolea taarifa (Contact Reporting Form)
e. Fomu ya majumuisho ya taarifa ya ufuatiliaji wa watu waliokuwa karibu na mgonjwa wa CORONA (Contact Field Summary Report Form)
f. Kipimajoto (Hand-held infrared thermometers or digital thermometers)
g. Vifaa vya kinga (barakoa na glovu) "gloves and mask"
h. Simu, Kishkwambi (Ipad), komputa mpakato (Lap top)
i. Vyombo vya usafiri

# 3 MAJUKUMU YA WASIMAMIZI

## 3.1 AFISA MTENDAJI WA MTAA/KIJIJI

a. Kuhakikisha anapatiwa rejista yenye orodha ya watu waliokuwa karibu na mgonjwa kulingana na sehemu yake husika
b. Kufuatilia iwapo mtu huyu anatimiza masharti kama alivyoshauriwa ili kupunguza maambukizi kwa wengine (Kipengele namba 4)
c. Kutunza siri za watu wanaofuatiliwa
d. Kusimamia ujazaji wa fomu ya masharti ya kuzingatia wakati wa kujitenga **(Kiambatanisho B)**
e. Kuchukua hatua stahiki chini ya Sheria ya Afya ya Jamii ya 2009.

## 3.2 AFISA WA AFYA MSIMAMIZI

a. Kuhakikisha kuna rejista yenye orodha ya watu waliokuwa karibu na mgonjwa **(Contact list)** kulingana na Wilaya/Halmashauri
b. Kuhakikisha uwepo wa rosta yenye orodha ya majina ya wafuatiliaji **(Contact tracers)** wa kila Wilaya/Halmashauri
c. Kuhakikisha watu wote waliokuwa karibu na mgonjwa wanapimwa joto la mwili angalau mara moja kwa siku
d. Kuhakikisha fomu zote za ufuatiliaji zimejazwa kwa ukamilifu
e. Kutoa taarifa ya majumuisho kwa Afisa wa Afya wa Wilaya saa kumi na mbili jioni kila siku.
f. Kuwasilisha orodha ya wasiofuata utaratibu wa ufuatiliaji ili wachukuliwe hatua
g. Kuhakikiksha kuwa utakasaji unafanyika kwa maeneo yote yaliyokuwa karibu au kupitiwa na mgonjwa wa COVID 19.

### 3.3 AFISA USTAWI WA JAMII/MAENDELEO YA JAMII

a. Kufuatilia, kubaini na kutatua changamoto zinazo husiana na ufuatiliaji
b. Kutoa ushauri nasaha na elimu kuhusu umuhimu wa kujitenga inapobidi

### 3.4 AFISA UFUATILIAJI MAHSUSI (CONTACT TRACER)

a. Kuhakikisha kuwa contact anapimwa joto la mwili. Aidha kwa siku ya kwanza ya kutembelewa, atapimwa joto la mwili kwa kutumia "**hand held infrared themorscanner**" kwa umbali wa mita 1 kutoka kwa mtu huyu anayepimwa. Namna ya kupima joto
    (i) Endapo atapimwa kwa kutumia hand held scanner, Mpimaji ataelekeza kipima joto kwa kunyoosha mkono kuelekea kwa contact kwa umbali kuanzia sentimita 3-5
    (ii) Endapo mtu huyu atatumia kipima joto chake cha kidigitali (digital thermometer) aelekezwe kuwa atoke nacho nje na ajipime ukimshuhudia.
    (iii) Kwa kipima joto ambacho si cha kidigitali; kitikiswe hadi kioneshe nyuzi joto 36, ndipo kiwekwe katikati ya kwapa na kibanwe kwa muda wa dakika moja hadi tano ndiyo kisomwe.
    (iv) Joto na dalili nyingine zirekodiwe katika fomu ya ufuatiliaji ya kila siku (Daily Contact follow up form).
    (v) Ikiwa joto litazidi nyuzijoto 37.5 au akiwa na dalili nyingine, taarifa itolewe mara moja kwa msimamizi na hatua stahiki zichukuliwe kwa mujibu wa miongozo iliyopo.
b. Kuwapatia contacts namba ya simu ya kupiga bila malipo ambayo ni "**199**" aweze kutoa taarifa endapo patatokea dharura
c. Kuhakikisha kuwa kuna majumuisho ya siku ***(Daily contact follow up)*** na yaingizwe katika fomu ya majumuisho ya kazi ***(Field Summary Report Form)***

## 4 TARATIBU ZA KUFUATA

a. *Contact* atatakiwa kufuata masharti yote atakayopewa pamoja na kujaza fomu ya ridhaa
b. *Contact* anatakiwa kuelimishwa namna ya kuzuia maambukizi wakati wote watakapokuwa ndani ya ufuatiliaji.
c. *Contact* atalazimika kunawa mikono na maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono vinavyothibitishwa na mamlaka za udhibiti.
d. Contact atalazimika kuvaa barakoa wakati wote wa ufuatiliaji

9

e. Watu wa nje watazuiwa kuwatembelea contacts kwa muda wote watakapokuwa wamejitenga
f. Contact wapewe huduma za chakula na mahitaji mengine bila kugusana au kukaribiana na mtoa huduma
g. Huduma kwa contacts wenye ulemavu zitatolewa kwa kuzingatia aina ya ulemavu walio nao
h. Inapowezekana contact afanye usafi mwenyewe ndani ya chumba chake.
i. Contact aliyejitenga akionesha dalili atamjulisha mfuatiliaji (contact tracer) kwa simu au kwa kupiga simu 199, na kupewa maelekezo ya kituo gani cha karibu cha kwenda kufanyiwa tathmini

## 5 UTARATIBU WA UKOMO WA UFUATILIAJI WA CONTACT

Ufuatiliaji wa contact utakoma pale ambapo atakuwa amefuatiliwa kwa siku 14 bila kuonesha dalili yoyote ya maambukizi. Yafuatayo yatafanyika kabla ya kuruhusiwa:

a. *Contact* atapewa uthibitisho wa maandishi kuwa ametimiza muda wa kujitenga
b. *Contact* atapewa elimu ya kuendelea kujikinga na ugonjwa wa Corona
c. Chumba kilichotumiwa na contact kisafishwe kabla ya kuanza kutumika na mtu mwingine

**NB: Mwongozo huu utakuwa ukifanyiwa marekebisho kulingana na mabadiliko ya hali ya ugonjwa nchini.**

Prof. Abel N. Makubi
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**

*Kiambatanisho A*

## Dodoso la tathmini ya mahali anapoishi mtu aliyekuwa karibu na mgonjwa wa COVID-19 (CONTACT)

Dodoso hili linalenga kufanya tathmini ya nyumbani kwa **mtu aliyekuwa karibu na mgonjwa (Contact) wa COVID-19** na kushauri namna gani mtu huyu atakaa nyumbani kwake au katika sehemu atakayoainisha yenye vigezo tajwa.

*Yafuatayo ni mambo muhimu ya kutathmini mahali anapoishi mtu aliyekuwa karibu na mgonjwa wa COVID-19*

| Na | Maelezo | Alama | Alama alizopata |
|---|---|---|---|
| 2.1 | Je, kuna uwezekano wa kupata chumba cha peke yake chenye choo? | Ndiyo - 5<br>Hapana - 0 | |
| 2.2 | Je kuna uwepo wa mahitaji muhimu ya kufanyia usafi kama maji na sabuni? | Ndiyo - 5<br>Hapana - 0 | |
| 2.3 | Je, kwenye nyumba kuna wazee, au watu wenye magonjwa sugu? | Ndiyo - 0<br>Hapana - 5 | |
| 2.4 | Je chumba kina mzunguko wa hewa wa kutosha ? | Ndiyo - 3<br>Hapana - 0 | |
| 2.5 | Je ana chumba cha kukaa peke yake? | Ndiyo - 2<br>Hapana - 0 | |
| 2.6 | Je, hali ya kiuchumi ya mtu aliyekuwa karibu na mgonjwa anaweza kumudu chakula kwa muda wa siku 14? | Ndiyo - 2<br>Hapana - 0 | |
| 2.7 | Je hali ya Usafi wa mazingira na ndani ya nyumba inaridhisha? | Ndiyo - 2<br>Hapana - 0 | |
| 2.8 | Je anatumia pombe, madawa ya kulevya au kilevi kingine chochote? | Ndiyo - 0<br>Hapana – 2 | |
| 2.9 | Je anaonekana kuaminika kuwa atatekeleza maelekezo atakayopewa? | Ndiyo - 2<br>Hapana – 0 | |
| | **Jumla ya alama** | **28 (100%)** | |

***Tathmini na kushauriana na mtu huyu, kwa kuzingatia vigezo tajwa.*** *Kumbuka eneo zuri ni lile lenye kupata alama 24 (asilimia 85%) au zaidi ya maswali yote hapo juu, ikiwemo vipengele 2.5 na 2.9 ni lazima viwepo. Aidha kama alama hazi hazipo, atalazimika kutafuta sehemu yenye vigezo hivyo kwa gharama zake.*

*Kiambatanisho B*

**Fomu ya Makubaliano kati ya Mtu aliyekuwa karibu na Mgonjwa wa COVID-19 (Contact) na Serikali kupitia Maafisa husika**

## 1. SAINI YA KUKUBALI KUZINGATIA VIGEZO NA MASHARTI YA KUFUATILIWA UKIWA NYUMBANI

Mimi Bw/Bi. ______________________________nakubali kufuata masharti, vigezo na maelekezo yote nitakayopewa wakati wa kufuatiliwa nikiwa nyumbani, kama mwongozo wa Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009, inavyoelekeza. Ninatambua kuwa ukiukwaji wa masharti haya utapelekea kuchukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria hii ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 mimi pamoja na shahidi wangu.

Saini______________________________Tarehe________________

**Jina la shahidi:** ______________________________

Saini: ______________________________Tarehe: _____

## 2. IDHINI

Tumejiridhisha/hatujajiridhisha kuwa Bw./Bibi ______________________________anaweza kufuatiliwa nyumbani:

1. Jina la Afisa wa Afya Msimamizi/Maendeleo ya Jamii
   Tarehe_______ Cheo ____________Saini__________
   Halmashauri ya ___________________________________

2. Mganga Mkuu wa Wilaya
   Ninakubaliana/Sikubaliani na tathmini
   Jina _____________
   Tarehe _______________________Saini____________
   Halmashauri ya ___________________________________

**Kiambatisho na. C**

**Mfano wa Barua ya Ruhusa**

**LOGO ya Halmashauri husika**

**Kwa yeyote anayehusika**

**YAH: UTHIBITISHO WA KUMALIZA SIKU 14 ZA UFUATILIAJI BAADA YA KUWA KARIBU NA MGONJWA WA COVID-19**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu

Mnamo tarehe …………, Ndugu ……………………………………… aliwekwa kwenye utaratibu wa kujitenga (Self quarantine) baada ya kubainika kuwa kwenye mazingira ya kuwa karibu na mgonjwa wa ugonjwa wa COVID-19.

Hadi kufikia tarehe ………., mtajwa huyu amemaliza siku 14 akiwa chini ya ufuatiliaji wa wataalamu wa Afya na hakuonesha dalili zozote za ugonjwa huo.

Hivyo, ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya imejiridhisha kuwa mtajwa huyu yupo salama na ameruhusiwa kuendelea na shughuli zake. Tunatoa rai apewe ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake.

Nashukuru kwa ushirikiano

---------------------------------

**Afisa Mtendaji wa Mtaa**

**Nakala:**

Mkurugenzi wa Halmashauri

Katibu Tawala wa Wilaya